## 1.2 KISWAHILI (102)

### 1.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

1 ***Insha ya lazima.***

Wewe kama mwanafunzi umepata nafasi ya kumhoji Mkurugenzi wa Habari nchini kuhusu umuhimu wa magazeti kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Andika mahojiano hayo.

2 "Magari ya matatu yameleta faida nyingi hapa nchini kuliko hasara." Jadili.

3 Pele hupewa msi kucha.

4 Andika insha itakayomalizika kwa:

"Niliipapia ile bilauri ya maji kwa pupa. Sikuwa na uhakika kuwa kiu yangu ingekatika. Nikapiga mafunda mawili, matatu. Baada ya kugumia bilauri yote, ndipo nilipotambua kuwa kweli maji ni uhai."



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

## 1.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

### 1 UFAHAMU (Alama 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Changamoto kubwa inayowakabili watu wengi katika mataifa yanayoendelea ni suala la chakula. Suala hili linaweza kuangaliwa katika sawia mbili tofauti. Kuna tatizo linalofungamana na uhaba wa chakula chenyewe. Uhaba huu unaweza kutokana na utegemezi mkubwa kwa zaraa kama nyenzo kuu ya uzalishaji wa chakula.

Zaraa katika mataifa mengi hususan yanayoendelea, hutegemea mvua. Kupatikana kwa mvua huathiriwa na mabadiliko ya tabianchi ulimwenguni. Matendo na amali za watu kama ukataji wa miti na uchafuzi wa mazingira huwa na athari hasi kwenye tabianchi hiyo. Mabadiliko ya tabianchi huweza kuvyaza ukame kutokana na **ngambi ya mvua**.

Kibinimethali hutokea wakati mafuriko yanapotokea na labda kuyasomba mazao mashambani na kusababisha baa la njaa. Hali hizi mbili husababisha matatizo makubwa ya chakula na kuathiri pakubwa suala zima la usalama wa chakula. Ili kuzuia uwezekano wa kuwepo kwa shida hii, pana haja ya kuwepo kwa mikakati na sera za kuhakikisha kuna usalama wa chakula. Kwa mfano, pana haja ya kukuza kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka **adha** inayosababishwa na ukosefu wa mvua. Kwa upande mwingine, sharti zichukuliwe hatua mufidi za kuzuia na kupambana na athari za gharika.

Changamoto nyingine inahusiana na usalama wa chakula chenyewe. Chakula kilichosibikwa na vijasumu au kwa njia nyingine ile huweza kumdhuru anayehusika. Msibiko wa chakula unatokana na vyanzo tofauti. Mathalan, uandalizi wa chakula kilichochafuliwa na choo, kutozingatia mbeko za usafi, uandaaji wa chakula na kukiweka katika hali ya uvuguvugu kabla ya kukipakua - hali inayochochea ukuaji wa viini na ulaji wa chakula kisichoandaliwa vyema.

Ili kuepuka uwezekano wa kuadhirika, pana haja ya kuzingatia usafi wa chakula na uandalizi unaofaa. Fauka ya hayo, vyombo vya uandalizi viwe safi, kanuni za usafi zifuatwe, upikaji na uandaaji uwe kamilifu. Hali hii isipozingatiwa, siha za raia wenyewezitaathirika pakubwa.

Maswali

(a) Taja aina **mbili** za kuangalia suala la chakula katika mataifa yanayoendelea. (alama 2)

(b) Taja hatua **mbili** zinazoweza kuchukuliwa kupambana na tatizo la chakula. (alama

(c) Eleza jinsi **nne** tofauti namna chakula kinavyoweza kuwa si salama? (alama

(d) Kwa nini inahalisi kukipakua chakula baada ya kukiandaa tu? (alama 1

(e) Ni mapendekezo gani anayoyatoa mwandishi kuhakikisha kuwa chakula kinafaa? (alama 4

(f) Eleza maana ya maneno haya jinsi yalivyotumiwa: (alama 2

(i) Ngambi ya mvua ........................................................................................

(ii) Adha ........................................................................................



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

## 2 MUHTASARI

Uwazaji tunduizi ni tendo ambalo huhusisha matumizi ya akili. Uwazaji huu umekitwa kwenye matumizi ya michakato kama makini, upangiliaji, uteuzi na tathmini. Hata hivyo, uwazaji huu si mchakato mwepesi bali ni mchakato changamano.

Mchakato wa uwazaji tunduizi unahusisha stadi na mikabala tofauti. Mathalan, kuweza kutambua na kubainisha misimamo ya watu wengine, hoja wanazozua na uamuzi waliofikia, kutathmini au kupima ushahidi uliopo ili kubainisha mitazamo tofauti. Vilevile, uwazaji tunduizi hushirikisha kupima hoja za upinzani na ushahidi uliopo kwa njia ya haki pamoja na kutambua yaliyofichwa au ukweli uliofunikwa na taswira ya juu juu. Hali kadhalika, uwazaji tunduizi hujumuisha kutambua mbinu zinazotumiwa kufikia misimamo fulani kwa mvuto zaidi na kwa matumizi ya mbinu za kishawishi. Aidha, uwazaji huu huhitaji kutathmini masuala kwa mtindo ulio wazi, kufikia uamuzi kama hoja zinazotumiwa zina mashiko au zinakubalika kuwa nzuri. Zaidi ya hayo, uwazaji tunduizi unahusisha kuwasilisha mtazamo kwa njia yenye uwazaji mzuri na inayoshawishi.

Uwazaji tunduizi una manufaa anuwai. Mosi, unasaidia kujenga makini ya utendaji. Pili, hupevusha uwezo wa usomaji kwa kuufanya usomaji huo uwe na malengo wazi. Fauka ya hayo, unamsaidia mtumiaji kutambua hoja kuu katika matini au ujumbe fulani bila ya kuzongwazongwa na hoja duni za pembeni. Uwazaji huu unasaidia kuuchonga uwezo wa kuikabili au kuiitikia hali fulani na kukuza stadi za uchanganuzi. Mwanadamu huwa mtu tofauti na bora anapoujenga na kuuimarisha uwazaji tunduizi wake.

Maswali

(a) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwanzo.
(Maneno 70 - 80) (alama 10; alama 2 za utiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

(b) Andika kwa muhtasari mambo muhimu katika aya ya tatu.
(Maneno 35 - 40) (alama 5; alama 1 ya utiririko)

**Matayarisho:**

**Nakala safi:**

## 3 MATUMIZI YA LUGHA.

(a) Tumia mzizi '- enye' katika sentensi kama:

(i) Kivumishi ..........................................................................................

(ii) Kiwakilishi ..........................................................................................

(alama 2)

(b) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa:-

Paka mweupe amenaswa mguuni. (alama 2)



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

(c) Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo:-

(i) Kiyeyusho ..............................................................................................

(ii) Kimadende..............................................................................................

(alama 1)

(d) Onyesha shamirisho kitondo, kipozi na ala katika sentensi ifuatayo:-

Kipkemboi alimbebea mwalimu mzigo kwa gari. (alama 3)

(e) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.

Maria alipika taratibu huku mama akimwelekeza vizuri. (alama 4)

(f) Nomino 'furaha' iko katika ngeli gani?

.............................................................................................................. (alama 1)

(g) Andika kinyume cha sentensi:

Watoto wameombwa waanike nguo. (alama 2)

(h) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa.

Mama alishangilia arusi ya mwana.

Anza: Mwana .............................................................................................. (alama 2)

(i) Tumia kirejeshi 'O' katika sentensi ifuatayo:-

Mtu ambaye hutupa tope hujichafua mwenyewe. (alama 2)

(j) Kanusha sentensi ifuatayo:

Mgonjwa huyo alipona na kurejea nyumbani. (alama 2)

(k) Ainisha vihusishi katika sentensi:

Ame aliwasili mapema kuliko wengine halafu akaondoka. (alama 2)

(l) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno "chuma". (alama 4)

(i) ..............................................................................................

(ii) ..............................................................................................



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

(m) Unda nomino kutokana na kitenzi 'tafakari' ................................................ (alama 1)

(n) Eleza maana mbili za sentensi:

Tuliitwa na Juma ........................................................................................ (alama 2)

(o) Ainisha viambishi katika kitenzi:-

Tutaonana........................................................................................ (alama 2)

(p) Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi cha kinyume. (alama 2)

(q) Huku ukitoa mifano eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)

(i).......................................................................................................................

(ii) .......................................................................................................................

(r) Akifisha kifungu kifuatacho:

Mzee alimwambia mwanawe njoo nikupeleke kwa babu yako angalau umjue mtoto aliuliza nani babu? (alama 4)

**4 ISIMUJAMII**

(a) Bainisha changamoto **tano** zinazoikabili lugha ya Kiswahili kama somo katika shule za upili nchini Kenya. (alama 5)

(b) Eleza namna **tano** za kukabiliana na changamoto ulizobainisha hapo juu. (alama 5



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

## 1.2.3 Kiswahili Paper 3 (102/3)

### SEHEMU A: TAMTHILIA

**KITHAKA WA MBERIA**: *Kifo Kisimani*
***Swali la lazima***

1 "Alijiona pwagu. Lakini Butangi ina pwaguzi pia."
Eleza tofauti baina ya wahusika wanaorejelewa. (alama 20)

### SEHEMU B: RIWAYA

**S.A. MOHAMED**: *Utengano*
***Jibu swali la 2 au la 3***

2 Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa riwaya ya Utengano:

(i) Kwelikinzani
(ii) Sadfa. (alama 20)

3 "Uhuru alioutaka na ulimwengu alioufahamu Maimuna umemdhuru hatimaye."
Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano **kumi.** (alama 20)

### SEHEMU C: USHAIRI

***Jibu swali la 4 au la 5***

4 **KUJITEGEMEA**

1 Nchi ni ile ambayo, imekita ardhini
Siyo ile iombayo, **ghaibu** na majirani
Taratibu siyo hiyo, wanachi twambizaneni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

2 Chumo lote na mitaji, leo limo maganjani
Bepari na wanyonyaji, wasalie maguguni
Shime utekelezaji, vingine havifanani
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

3 Twaishije tujihoji, wanachi humu nchini
Kila tunachohitaji, kupatakwe ugenini
Hiyo ni tete haviji, tongo tupangusaneni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

4 Kuomba wataalamu, ni mwendo haulingani
Tupate wa humu humu, wajuzi wa kila fani
Mbele washike hatamu, kwa mapimo na makini
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji



Powered by: manyam franchise
www.manyamfranchise.com

5 Tuufuate wongozi, pamwe na nyingi imani
Tushiriki kila kazi, na mambo yalomkini
Mikopo ina kinyezi, si kitu cha tumaini
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

6 Yote hatuyatimizi, alotimiza ni nani
Lakini tuwe maizi, tusizurure mijini
**Tukamshabihi** kozi, kipanga au kunguni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

7 Shujaa itakiwavyo, aonekane vitani
Na sisi vita tunavyo, roho kwa roho ugani
'Kutegemea' vilivyo, kondo tujiamueni
Daima hukaa chini, maganja ya mpewaji

***Boukhet Amana: Malenga wa Mrima***
Mwinyihatibu Mohammed
Oxford University Press
1977

(a) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)

(b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu moja. (alama 2)

(c) Eleza mambo **matatu** ambayo mshairi anashauri nchi ifanye ili kujitegemea. (alama 3)

(d) Taja aina moja ya idhini ya kishairi iliyojitokeza kwa wingi zaidi katika shairi na utoe mifano mitano ya matumizi yake. (alama 7)

(e) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi:

(i) Ghaibu

(ii) Tukamshabihi.

(alama 2)

5 **HAKI**

1. Haki watutisha, tusikuandame, kwa matendo yetu,
Watukorofisha, tusikuandame, kila penye kitu,
Mbona watugwisha, miba ituchome, kwenye huu mwitu,
Tutokwe na utu!



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

2. Hatutakufanya, mwana kwa mvyele, aliyemzaa,
Haki watunyima, machumi ya mbele, na nyingi hadaa,
Tuchumayo nyanya, uchungu umbele, hatuna wasaa,
Haki twashangaa!

3. Na kambi nzima, kunaiyenea, hasa hapa petu,
Tunakutazama, kwa kuulizia, kuweza thubutu,
Na kwenye milima, ilotueka, kupandia watu,
Usifanye katu!

4. Sio hao mabwana, waloteuliwa, kupata mwangaza,
Haki wakubana, lilotarajiwa, kwenye hichi kiza,
Ndevu kuchomana, wengine kuliwa, tukijiingiza,
**Kambi yatuviza**!

5. Haki huna njia, kizuizi mali, ndio njia panda,
Tukiifatia, hatufiki mbali, wengi tunaganda,
Sio yetu nia, lakini akili, mali ishapenda,
Haki yatuponza!

6. Wala hutasemwa, sababu ni nyoyo, kwisha haribika,
Ya mali kuchumwa, vyovyote iwavyo, itavyopatika,
Wakati mtumwa, ushatumwa ndivyo, na ushatufika,
Kwetu ni mashaka!

7. Haki hufanyiki, papitapo mambo, na vikubwa visa,
Watu hawataki, kutenda kijambo, tunu yao pesa,
Sisi kwetu dhiki, yatunisha tumbo, wao hata hisa,
Na ndio ya sasa!

8. Haki husimami, kwa viumbe sisi, tuvyojaaliwa,
Na huna ulimi, **kuweza tukisi**, tukageukiwa,
Zama za uchumi, zishashika kasi, nguvu zishapewa,
Haki wauliwa!

9. Iwe hivi haki, hakuna mmoja, akukumbukae,
Hatuna ashiki, kuvuta la haja, haki ituvae,
Mbona hatutaki, twalia na tija, haki iambae,
Haki tamati!

**Suleiman A. Ali:**
***Malenga Wapya***

(a) Eleza dhamira ya shairi hili. (alama 2)



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

(b) Huku ukitoa mfano, eleza aina ya shairi hili. (alama 3)

(c) Taja na ufafanue tamathali ya usemi inayotawala katika shairi hili. (alama 3)

(d) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina tatu za idhini ya kishairi katika shairi hili. (alama 6)

(e) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Mshairi ana maana gani kwa kusema:

(i) Kambi yatuviza

(ii) Kuweza tukisi.

(alama 2)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**K.W. WAMITILA:** *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyinginezo*

***Jibu swali la 6 au la 7***

**6** "Cheche ndogo hufanya moto mkubwa."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua maudhui **manne** yanayohusiana na chanzo cha tukio linalorejelewa katika dondoo hilo. (alama 8)

(c) Eleza matokeo **manne** ya tukio linalorejelewa katika dondoo. (alama 8)

**7** "Mganga na wateja wake wote walikosa busara." Fafanua ukweli wa kauli hii kwa mifano **kumi** kutoka hadithi ya 'Siku ya Mganga.'

(alama 20)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8** (a) Eleza maana ya malumbano ya utani. (alama 2)

(b) Bainisha sifa **nne** za malumbano ya utani. (alama 8)

(c) Fafanua majukumu **matano** ya malumbano ya utani katika jamii. (alama 10)



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

**MAUDHUI**

**Umuhimu ushirikishe**:

- Magazeti ni nyenzo za kutolea mafunzo kwa wanafunzi. Kuna makala mengi ya kielimu yanayoweza kuwanufaisha wanafunzi.
- Huweza kufahamisha kuhusu mambo na matukio hapa nchini na nje ya nchi.
- Ni chombo cha kuburudisha na kuondoa uchovu wa kiakili. Makala ya michezo kama vile kujaza mraba, na soduku huweza kuburudisha.
- Kwa mfano kupitia kwa tahariri na baarua kwa mhariri
- Magazeti huwapa wanafunzi nafasi za kubadilishana mawazo, changamoto na tajriba zao, kwa mfano kupitia kwa tahariri na barua kwa mhariri.
- Hushirikisha makala kuhusu utamaduni na hivyo kuwapa vijana njia ya kuwasilisha au kujifunza kuhusu utamaduni wao.
- Matangazo ya kazi huwajuza watu kuhusu nafasi za kazi,
- Hufunza maadili
- Kukuza hamu ya kupenda kusoma
- Baadhi huwa na maswali ya mitihani ambayo huwasaidia wanafunzi kudurusu.
- Kukuza hamu ya kuwa waandishi
- Kuna zawadi kwa wanaojibu maswali

Kukuza ubunifu makala kama vile tahariri huweza kuwaonyesha wanafunzi namna ya kutumia insha kwa upeo wa juu na kwa ukakamavu.

Katika hitimisho, mhoji amwuulize mhojiwa kutoa ushauri wake kwa wanafunzi wa shule za sekondari kuhusiana na umuhimu wa magazeti kwao.

Mahojiano yahitimishwe kwa mhoji kumshukuru mhojiwa na kuagana.

**Vipengele vikuu ambavyo lazima vibainike**

Kichwa
Utangulizi
Mwili
Muundo - Tamthillia/mtindo wa mazungumzo
Hitimisho

2. Insha hii ni ya mjadala. Mtahiniwa aonyeshe hoja za kuunga mkono na kupinga. Hoja ziweze kutetewa kwa ithibati. Kisha mtahiniwa ahitimishe kwa kuonyesha msimamo wake.

**Muundo**
Sehemu zifuatazo zijitokeze:

**Utangulizi**
Sehemu hii ionyeshe hoja za kijumla kuhusu magari ya matatu.

**Mwili**
Hoja zijadiliwe hapa. Tazama mifano.



Powered by: manyam franchise
www.manyamfranchise.com

**Hoja za Kuunga mkono**

- Husaidia watu wengi ambao hawajamiliki aina yoyote ya vyombo vya usafiri kusafiri kwa wepesi.
- Yameweza kutoa nafasi nyingi za kazi; kuanzia kwa wawekezaji, madereva, utingo, manamba, wauza vipuri vya magari na hata wanaoyatengeneza yakiharibika.
- Huweza kujaa haraka yakilinganishwa na mabasi ambayo huchukua muda mrefu kujaa.
- Huweza kupatikana kwa urahisi katika sehemu nyingi nchini iwe mijini au mashambani.
- Wawekazaji wameweza kutajirika kutokana na uwekezaji wa biashara hii.
- Ni biashara ambayo inaipa serikali kodi kubwa/mapato.

**Hoja za kupinga**

- Matatu husababisha ajali nyingi zaidi humu kuliko magari mengine.
- Ajali kutokana na matatu husababisha madhara mengi zaidi kama vile vifo vingi, majeruhi, kulemazwa kwa wingi, na hasara za kiuchumi.
- Mashirika mengi ya bima hupata hasara kubwa kutokana na magari ya matatu na mengi hufilisika na kufunga biashara.
- Biashara ya matatu huhimiza watu wengi kuwa wavivu, mathalani, mtu hawezi akatembea masafa mafupi hata kama aendako ni karibu kwa sababu magari ya matatu yako tele.
- Biashara ya matatu imehusishwa na uzorotaji wa maadili ya kijamii. Wahudumu katika sekta hii wamehusishwa na utumiaji na usafirishaji wa vileo kama afyuni, pombe haramu na kushiriki katika usherati.
- Magari ya matatu husababisha msongamano barabarani hasa katika sehemu za mijini.
- Magari ya matatu yamechangia katika uchafuzi wa mazingira kutokana na kelele za utingo, manamba na upigaji wa honi pamoja na moshi.
- Biashara ya matatu imepotosha vijana wengi ambao wanavutiwa na kukimbilia biashara hii badala ya kuendelea na shuguli kama vile masomo yanayoweza kuwasaidia maishani pakubwa kuliko biashara hii.

**Hitimisho**: Mtahiniwa aonyeshe msimamo wake kwa kueleza anaegemea katika kupinga au kuunga mkono.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

3. Hii ni insha ya methali. Methali hii ina maana kuwa upele hupewa mtu asiye na kucha kwa kuwa hana uwezo wa kujikuna. Maana ya ndani ya methali hii ni kwamba matatizo humkumba mtu ambaye hana ujuzi/uwezo /mbinu za kuyatatua.

Pele - Matatizo yanayomkumba mtu akakosa namna ya kuyatatua.
Kucha - uwezo /mbinu/njia za kutatua matatizo /ujuzi
Mtahiniwa aandike kisa kinachodhihirisha:

- Mtu asiye na ujuzi wa jambo akiwa amepatikana na jambo hilo na hajui namna ya kulitatua.

Au

- Mtu mwenye kitu ambacho hakihitaji ilihali anayekihitaji hakipati.

Au

Mtu ambaye ana uwezo na hali hapatwi na matatizo lakini yule asiye na uwezo anapatwa nayo.

4. Hii ni insha ya mdokezo. Mtahiniwa aandike insha yenye kisa ambacho kinaonyesha akihangaika kwa kiu ya maji. Baada ya mahangaiko haya na kupata bilauri moja ya maji ndipo anapotambua umuhimu wa maji.

Yafuatayo yafuatwe katika kutuza swali hili.

- Mtahiniwa aeleze hali ya kukosa maji.
- Aeleze kilichotendeka kabla ya kupata maji.
- Ajihusishe katika kisa.
- Asiyejihusisha - amejitungia swali.
- Ahusike katika hali ngumu ya kuhitaji maji.
- Asiponukuu maneno aliyopewa, amejitungia swali.
- Akinukuu sehemu ya maneno amejitungia swali.
- Akiongeza sentensi moja, mbili au kifungu amejitungia swali.
- Akiongezea maneno hadi matano aondolewe alama 2 baada ya kutuzwa.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

## 7.2 Kiswahili Karatasi ya 2 (102/2)

UFAHAMU

(a) (i) Uhaba wa chakula/Ukosefu wa chakula/Upungufu wa chakula

(ii) Usalama wa chakula chenyewe

(Hoja 2 x 1 = 2)

(b) (i) Kuwepo kwa mikakati ya kuhakikisha kuna usalama wa chakula/kukuza kilimo cha umwagiliaji ili kuepuka adha inayosababishwa na ukosefu wa mvua/zichukuliwe hatua mufidi za kuzuia na kupambana na athari za gharika.

(ii) Kuwepo kwa sera za kuhakikisha kuna usalama wa chakula

(Hoja 2 x 1 = 2)

(c) (i) Uandalizi wa chakula kilichochafuliwa na choo;

(ii) Kutozingatia mbeko za usafi;

(iii) Kukiandaa chakula na kukiacha katika hali vuguvugu kabla ya kukipakua;

(iv) Ulaji wa chakula kisichoandaliwa vyema.

(Hoja 4 x 1 = 4)

(d) Kuzuia hali inayochochea ukuaji wa viini/kuhakikisha kuwa chakula hakitakuwa na viini

(e) (i) Pana haja ya kuzingatia usafi wa chakula;

(ii) Uandalizi unaofaa;

(iii) Vyombo vya undalizi viwe safi;

(iv) Kanuni za usafi zifuatwe;

(v) Upikaji na uandalizi uwe kamilifu. (Hoja 4 x 1 = 4)

(f) (i) Ngambi ya mvua –Uhaba, upungufu, shida, ukosefu, uchache

(ii) Adha – Shida, kero mashaka, usumbufu, dhiki, matatizo, taabu, janga

(Hoja 2 x 1 = 2)

- Kuadhibu

(i) Ondoa alama 3 za makosa ya hijai yanapotokea kwa mara ya kwanza, yaani □ alama hadi kufikia makosa 6.

(ii) Ondoa ½ alama kwa kila kosa la sarufi kufikia ½ ya alama alizopata katika kila kisehemu.

2 MUHTASARI

(a) (i) Uwazaji tunduizi ni tendo ambalo huhusisha matumizi ya akili.

(ii) Umekitwa kwenye mizizi ya michakato kama makini, upangiliaji, uteuzi na tathmini.

Au

Umekitwa kwa mizizi ya michakato mbalimbali.

(iii) Uwazaji si mchakato mwepesi.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

Au

Uwazaji ni mchakato changamano

(iv) Uwazaji tunduizi unahusisha stadi na mikabala tofauti.
(v) Hushirikisha kupima hoja za upinzani na ushahidi uliopo kwa njia ya haki/ukweli uliofunikwa na taswira ya juu juu.
(vi) Hujumuisha kutambua mbinu zinazotumiwa kufikia msimamo fulani kwa mvuto zaidi na kwa matumizi ya mbinu za kishawishi.
(vii) Huhitaji kutathmini masuala kwa mtindo ulio wazi kufikia uamuzi.
(viii) Huhusisha kuwasilisha mtazamo kwa njia yenye uwazaji mzuri na inayoshawishi.


(Hoja 8 x 1 = 8)

(b) (i) Unasaidia kujenga makini ya utendaji

(ii) Hupevusha uwezo wa usomaji kwa kuufanya uwe na malengo wazi
(iii) Humsaidia mtumiaji kutambua hoja kuu katika matini/kutambua ujumbe fulani bila kuzongwazongwa na hoja duni za pembeni
(iv) Unasaidia kuuchonga uwezo wa kuikabili hali fulani/unasaidia kuitikia hali fulani.
(v) Unasaidia kukuza stadi za uchanganuzi.
(vi) Binadamu huwa mtu tofauti na bora anapojenga na kuuimarisha uwazaji tunduzi wake.

(Hoja 6 x 1 = 6)

- Mtindo wa kutuza




- Kuadhibu

Ondoa makosa 6 ya hijai yotokeapo mara ya kwanza kwa kuadhibu □ alama kwa kila kosa yaani alama 3
Ondoa alama 3 kwa makosa 6 ya mwanzo ya sarufi(s)
Ondoa alama 1 kwa ziada (z) ya maneno 10 ya mwanzo kisha endelea kuondoa □ alama kwa kila ziada ya maneno 5 hadi mwisho wa jibu lake

3 MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) Mfano – Mwanafunzi mwenye tabia nzuri hupendeza
(ii) Mfano - Mwenye gari amewasili
Mwenye kula kwa pupa hafaidi utamu
Amesema lenye maana

(Hoja 1 x 2 = 2)



Powered by: manyam franchise
www.manyamfranchise.com

(b)

- Paka jeupe limenaswa guuni.
- Jipaka jeupe limenaswa jiguuni.
- Paka jeupe limenaswa jiguuni.
- Jipaka jeupe limenaswa guuni.

(Alama 1 x 2 = 2)

(c) (i) /y/na/w
(ii) /r/
**(Alama □ x 2 = 1)**

**(d)** Kitondo – Mwalimu
Kipozi – Mzigo
Ala – Gari

(Alama 1 x 3 = 3)

(e)

| S | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S1 | | | U | S2 | | |
| KN | KT | | | KN | KT | |
| N | T | E | | N | T | E |
| Maria | alipila | taratibu | huku | mama | akimwelekeza | vizuri |

(Alama 4)

(f) 1-1

(Alama 1 x 1 = 1)

(g) (i) Neno watoto lisibadilike – Likibadilishwa ondoa □ alama
(ii) Wameombwa - Wameamrishwa
Wamelazimishwa
Wameshurutishwa
(iii) Waanike - Waanue

(Alama 2 x 1 = 1)

(h) Mwana alishangiliwa arusi na mama.
Mwana alishangiliwa arusi yake na mama.
Mwana alishangiliwa arusi na mamake.

(Alama 2 x 1 = 2)

(i) Mtu atupaye tope hujichafua mwenyewe.
Mtu anayetupa tope hujichafua mwenyewe.
Mtu atupaye tope ndiye ajichafuaye/mwenyewe.
Mtu anayetupa tope ndiye anayejichafua.
Mtu ajichafuaye mwenyewe ni yule atupaye tope.

(Alama 2 x 1 = 2)

(j) Mgonjwa huyo hakupona wala kurejea nyumbani.
Mgonjwa huyo hakupona na hakurejea nyumbani.
Mgonjwa huyo hakupona wala hakurejea nyumbani.
Mgonjwa huyo hakupona na kurejea nyumbani.

(Alama 2 x 1 = 2)

(k) Kuliko : Kihusishi kilinganishi
Halafu : Kihusishi cha wakati

(Alama 1 x 2 = 2)



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

(l) Chuma : Madini, mtu mwenye nguvu nyingi, tungua/tundua, tafuta mali.
* Sentensi zidhihirishe maana mojawapo ya hizo zilizoelezwa.

(Mbili zozote 2 x 2 = 4)

(m) Tafakuri, kutafakari, utafakari.

(Alama 1 x 1 = 1)

(n)
(i) Juma alituhitaji kwenda kwake.
(ii) Mimi pamoja na Juma tuliitwa na mtu fulani.
(iii) Sisi pamoja na Juma tuliitwa na mtu fulani.
(iv) Juma aliwaita watu wengine kwake.
(v) Watu wengine pamoja na Juma waliitwa na mtu fulani.

(Alama zozote 1 x 2 = 2)

(o) (i)

| | | |
|---|---|---|
| tu | - | Kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi |
| ta | - | Kiambishi cha wakati ujao |
| on | - | |
| an | - | Kiambishi cha mnyambuliko au kauli ya kutendana |
| a | - | Kiishio (kauli tenda) |

Au

(ii)

| | |
|---|---|
| tu)<br>ta) | Viambishi awali |
| an)<br>a ) | Viambishi tamati |

(alama 1 kwa kila kiambishi)
1 x 4 = 4

(p) Viunganishi vya kinyume - lakini, ijapokuwa, japo, ingawa, ila, bali, ilhali, hata kama/hata hivyo

(Alama 2 x 1 = 2)

(q)
(i) Irabu pekee – kwa mfano – o - a
(ii) Konsonanti pekee – kwa mfano – m tu
(iii) Konsonanti na irabu – kwa mfano ba – ba
(iv) Konsonanti konsonanti irabu – kwa mfano – mba-vu
(v) Kiyeyusho na Irabu wa-ya

(Mbili zozote, alama 1 x 2 = 2)

(r) Mzee alimwambia mwanawe, "Njoo nikupeleke kwa babu angalau umjue." Mtoto aliuliza, "Nani babu?"

(Alama 4)

4 ISIMUJAMII

(a)
(i) Kukua na kuenea kwa lugha ya Sheng'.
(ii) Watu wengi kutothamini lugha ya Kiswahili.
(iii) Watu wengine kutawaliwa na kasumba ya kigeni hadi kupenda Kiingereza na lugha zingine za kigeni na kudunisha Kiswahili.
(iv) Vyombo vya mawasiliano vinapotosha Kiswahili sanifu.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

(v) Shughuli nyingi shuleni zafanyika kwa Kiingereza.
(vi) Lugha ya Kiingereza kutumika kufunzia masomo mengi. Kiswahili kinafunza lugha ya Kiswahili tu.
(vii) Ukosefu wa walimu waliofuzu katika Kiswahili katika baadhi ya shule
(viii) Ukosefu wa vitabu katika baadhi ya shule
(ix) Vipindi vichche vya kufunza Kiswahili
(x) Uhaba wa wakaguzi na waelekezaji waliohitimu katika Kiswahili
(xi) Athari za lugha ya kwanza.
(xii) Kutohusishwa kwa lugha ya Kiswahili katika masuala ya kisayansi na teknolojia.

(zozote 5 x 1 = 5)

(b)
(i) Kuwahimiza vijana kutumia lugha mwafaka ya Kiswahili kutegemea muktadha
(ii) Kuwahimiza wanafunzi kukionea Kiswahili fahari
(iii) Kiswahili kiwe lugha rasmi na kitumiwe katika shughuli zote za kiserikali
(iv) Kuundwa kwa asasi ya kudhibiti matumizi mwafaka ya Kiswahili kwenye vyombo vya mawasiliano
(v) Sera bora za matumizi ya Kiswahili shuleni ili kukipa Kiswahili hadhi sawa na Kiingereza
(vi) Kuweka sera ambapo Kiswahili kitatumika kufundishia baadhi ya masomo kama vile dini, stadi za kimaisha, ujasiri na kadhalika
(viii) Serikali kuhakikisha kuwa imewaajiri walimu wa Kiswahili waliohitimu katika shule zetu zote
(ix) Mashirika ya uchapishaji yachapishe vitabu vingi kwa lugha ifaayo na kwa gharama nafuu
(x) Vipindi vya kufundishia Kiswahili viongezwe
(xi) Serikali ihakikishe kuwa kuna wakaguzi wa kutosha kukabiliana na idadi ya shule zinazozidi kuongezeka
(xii) Matumizi yafaayo ya lugha ya Kiswahili yahimizwe kuanzia shule za msingi
(xiii) Kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika masuala ya kisayansi na teknolojia

(zozote 5 x 1 = 5)

- Kuadhibu

(i) Ondoa ½ alama kwa kosa la hijai (h) litokeapo kwa mara ya kwanza hadi kufikia makosa 6; yaani alama 3 katika swali zima.
(ii) Ondoa ½ alama kwa kosa la sarufi(s) litokeapo mara ya kwanza hadi kufikia makosa 6, yaani alama 3 katika swali zima.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

# MWONGOZO WA FASIHI YA KISWAHILI. K.C.S.E 2011

## 1. KIFO KISIMANI (LAZIMA). SEHEMU YA A

Pwagu ndiye Mwelusi na pwaguzi ni Gege. Wahusika hawa ni watoto wa mama mmoja lakin walitofautiana. Mtahiniwa pia anaweza kutambulisha dondoo – Maneno haya yanasemwa na Gege kwa {Batu} kuhusu Mwelusi/ wanaorejelewa ni Mwelusi na Gege. (**maelezo**)

Pwanguzi pia anaweza kuwa Bokomo

| | **Mwelusi** | | **Gege** |
|---|---|---|---|
| i) | Alikuwa na **mitazamo** maalumu kuhusu maisha. Amezinduka k.m Anawachochea watu kususia mkutano. | i) | Alikuwa na mtizamo finyu kuhusu maisha / kwake maisha bora ni kuoa mke na kupata watoto wake mwenyewe. |
| ii) | Alifikiria hali ya **umma** wa Butangi/ mazingira; maji. | ii) | Fikira zake zilifungwa na mahitaji yake ya kibinafsi/ ya kimsingi k.v kuwvutia wasichana |
| iii) | Alikuwa na **msimamo** thabiti kuhusu mambo/ anakataa vishawishi vya Batu. | iii) | Alikubali kushawishiwa na Mweke na Talui akamuua Mwelusi. |
| iv) | Aliwa**heshimu** watu, mfano kumtaja Kaloo kwa jina la mama. | iv) | Aliwakosea watu heshima hasa mamake, anajibizana naye. |
| v) | Alikuwa na **mahusiano** mazuri na wanawake k.m Atega, walifanya kazi kwa pamoja/ uhusiano wa kisiasa. | v) | Aliamini maisha yalikuwa ni wanawake kumpɛ sifa/ raha na kuoa. |
| vi) | Alikuwa mwanaharakati aliyepigania **ukombozi** wa raia k.m kuteswa gerezani | vi) | Nia yake ni kujikomboa kiuchumi. |
| vii) | **Aliwajali** watu wengine/ kuhakikisha wanapata maji | vii) | Alijijali yeye mwenyewe/ ana ubinafsi. Anatengneza ala badala ya kwenda kumtembelea Mwelusi. |
| viii) | Alifahamu ukweli wa mambo kuhusu **haki** za wananchi/ alipinga utawala wa Bokono. | viii) | Aliunga mkono utawala wa Bokono. |
| ix) | **Mzalendo** – Anakataa kutoroka Butangi. | ix) | Ni mzalendo wa kijinga (Msaliti). Anausaliti udugu wake kwa Mwelusi kwa kumuua. |
| x) | **Jasiri** – hata anapoteswa gerezani anakataa kusema anampenda Bakono. | x) | Mwoga – anpoitwa na Mweke anadhani anaitiwa adhabu. |
| xi) | Mwenye **utu** – anawazia Butangi vyema (usalama, amani, maendeleo, chakula. | xi) | Katili – anamuua Mwelusi. |
| xii) | Mwenye maarifa/ **busara** – aligundua ujanja wa Batu alipomwambia atatuzwa. | xii) | Mjinga – alidanganywa kwa urahisi kuwa atamwoa Alida/ anakubali ahadi ambazo hajaziona. |
| xiii) | Mpenda mabadiliko/ mwana**mapinduzi.** | xiii) | Mhafidhina – anataka utawala wa Bokomo uendelee. |
| xiv) | **Mkweli** – Anamwambia Gege kuwa kuwaza kuwa maisha ni kuoa na kupata watoto ni kujitia katika kiwango cha nyani.. | xiv) | Mnafiki/ mwongo – anamdanganya mamake kuwa sasa hana kinyongo na Mwelusi. |



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

Maana ya Pwagu na Pwaguzi; ni kuwa kuna mwizi na kuna mwizi stadi. Pwagu hushindwa na pwaguzi; Bokono alimuua Mwelusi hatimaye ambaye alikuwa ndiye pwagu.**(maelezo)**

| **Mwelusi** | **Bokomo** |
|---|---|
| i) **Kujali** masilahi ya Wanabutangi . km kuhakikisha wamepata maji. | i) Kuwakandamiza. K.m. kuwanyima maji. |
| ii) Ni **Mzalendo** halisi. Anateswa gerezani lakini haikani Butangi. | ii) Ni msaliti/mzalendo hasi. Kutawala kwa mabavu. Wapende wasipende. |
| iii) Alijali **mazingira** . km ukataji miti, maji. | iii) Aliruhusu miti kukatwa na mmomonyoko wa udongo kuongezeka. |
| iv) Alipenda haki: wazalendo wapewe **maji**. | iv) Alikiuka haki za wanabutangi k.m. kumfungia Mwelusi gerezani. |
| v) **Mkweli**: anasema Butangi haiongozwi vyema. | v) Mwongo: anasema anapendwa, kina Batu wanasema sifa za uongo kumhusu. |
| vi) Heshima kwa wanawake. K.m. Alifanya **kazi** pamoja na Atega/ kisiasa. | vi) Ana jicho la nje k.m. kumtamani Kaloo; ana hawara; yule mwananke aliyepigwa na Nyalwe. |
| vii) **Jasiri**: kukataa kusema anampenda Bokono anapopigwa. | vii) Mwoga; anaota ndoto za kuzikwa akiwa hai; anaweka mikakati ya kumuua Mwelusi. |
| viii) Mwana**harakati** wa kukomboa nchi yake. Anataka Butangi yenye uswa kwa wote.isiyo na bughudha. | viii) Kukandamiza wananchi k.m. anatumia propaganda eti anapenda watoto na huku anagawa kiwanja chao cha kuchezea. |
| ix) Anajali masilahi ya **umma**. Anakubali kuteswa ili awakomboe. | ix) Anakataa kuwasikiliza raia. Anasema Mama Agoro asiende kumwona, anakubali uwanja wa watoto kuchukuliwa. |
| x) Angelitaka **haki** itendeke kwa kila mwanabutangi (usawa). | x) Angelipenda kuwafaidi wachache. Anawakinga wahalifu kama vile Askari II. |
| xi) Maarifa/ **busara** – aligundua ujanja wa Batu alipokuwa gerezani. | xi) Mjinga – alikataa/ pinga ushauri wa Nyalwe/ kuwa aache uongozi mbaya. |

## UTENGANO. SEHEMU YA B

**2) Kwelikinzani**

i) Kwelikinzani – **(maelezo)** mbinu ya kuonyesha maneno yanayojipinga yenyewe lakini ukichunguza yana ukweli fulani. Usahihishaji pia ulilkubali maelezo ya kinaya

ii) Maimuna kujifanya anachagua kuwa **huru** ilhali uhuru wenyewe haumsaidii. Anajikuta taabani hata akiwa nje ya kasri

iii) Maksuudi**kudai** awapenda na kuwajali wanajamii na familia kuwa awasaidia huku anawaibia na kuwatesa.

iv) Maksuudi kujifanya mwanadini muumini kiasi cha kwenda kwa **ibada** huku anatenda maovu (km usherati, ufisadi)

v) Kazija mwanzoni anachorwa kama kwamba anawa**chuki**a wanaume huku akiwa anajitayarisha kumpokea mmoja wao na hata anampokea Mussa papo hapo.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

vi) **Wanasiasa** wanadai kuwa wanajali umma: watawasaidia raia lakini walikuwa wanajitakia makuu – mfano Maksuudi/ Zanga.

vii) **Ndugu** wawili Inspekta Fadhili na Maksuudi/wanachorwa kuwa ndugu lakini mahusiano yanaonyesha kinyume. Damu hapo si nzito kuliko maji. Uk. 76 (kufukuzwa kwa Inspekta Fadhili/ makaribisho)

viii) Maksuudi kudai kuwa anampa Inspekta **pesa** za bure kuwa hamna kosa la kufichwa (makosa ya jinai) alikuwa na hatia.

ix) Kazija kumkaribisha Maksuudi na kusema mambo ni **shwari** lakini amempangia mabaya.

x) Biti Kocho kudai Maimuna ame**tafutwa** kote kote ilhali anajua alipo Maimuna.

xi) Farashuu kum**torosha** Maimuna na mwishowe Maimuna kuolewa na mjukuu wake Kabi.

xii) Maksuudi kukataa na **kitoto** eti kitakufa njaa na mwishowe kinafia kwake.

xiii) Maksuudi alipokuta kitoto kimezaliwa, badala ya kufurahia anam**chapa** na kumtaliki Tamima.

xiv) Kitoto cha Maksuudi kinapozaliwa ku**onjeshwa** shubiri na asali.

xv) Maimuna kuambiwa na Biti Kocho mapenzi ni kitu kizuri ilhali **mapenzi** ya wazazi wao ni majonzi.

xvi) **Dunia** ni kitu si kitu ….. Maneno ya mwandishi Maksuudi anapoenda pale hospitalini.

**Zozote 5 x 2 = 10**

**Sadfa**

i) (**Maelezo**) Kutokea kwa mambo mawili kana kwamba yamepangwa ilhali hakuna matayarisho wala maagano ya namna yoyote.

ii) Maksuudi kurejea nyumbani bila kutarajiwa kisha anapata **mtoto** amezaliwa (Bi. Tamima amezalishwa)

iii) Kazija kama mwanamke kuwepo **mkutanoni** kisha akainuka na kumwuliza maswali Maksuudi.

iv) Maksuudi hakutarajia kukutana na **Mussa** kule kwa Kazija, pia Mussa hakutarajia.

v) Mussa, Maimuna, Tamima na Maksuudi wanapokutana **mwisho**we.

vi) Maksuudi kukutana na Mussa akiwa **daktari**.

vii) Farashuu kukutana na Maimuna mara ya kwanza kule kwake wanapotafuta **Mkunga**.

viii) Farashuu akishuhudia kuchumbiana kwa Maimuna na **Kabi**./ Farashuu ndiye alimtorosha Maimuna na hakutarajia aolewe na Kabi.

ix) **Simu** kupigwa nyumbani mwa Maksuudi huku Inspekta Fadhili yupo na alikuwa anaendelea na uchunguzi.

x) Ku**sambaratika** kwa familia ya Maksuudi kutokea usiku mmoja.

xi) Rashid kuona **tangazo** gazetini kuhusu Maimuna kule Rumbalola wakati Maksuudi alikuwa anamtafuta.

xii) **Maulidi** kumsikia Maimuna akiimba na kumpa kazi ya uimbaji huko Rumbalola..

xiii) Bi. Tamima kushikwa na **uchungu** wa uzazi na Farashuu kuitwa kuwa mkunga.

xiv) Kabi **kukutana** na Maimuna Futoni na kupendana na kuoana ilhali wana uhusiano wa kutoka Liwazoni. (kihistoria).

xv) Maimuna kukutana na Kabi wakati anatafuta kitoweo na Kabi kumpa **samaki**.

xvi) Askari kufika kuwakamata Maksuudi na Zanga wakati tu **umati** umelipuka kutaka kuwaua.

xvii) Maimuna amechanganyikiwa na hajui pa kwenda anatokea **Dora** na kumwelekeza kwa Biti Sururu.

xviii) **Wimbo** wa Bantus kule Rumbalola – Nilikimbia kwa baba … uliimbwa wakati Maksuudi aliendа kumtafuta Maimuna hapo/Maimuna pia amekimbia kwa babake..

xix) Uchungu wa uzazi unampata Tamina mara tu Maksuudi anapoondoka nyumbani.

**Zozote 5 x 2 = 10**



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

**3) Uhuru alioutaka Mainuna**

i) Maimuna alijikuta aki**dhibiti**wa na watu wengine. Mfano Mama Jeni, Biti Sururu, James na Shoka.

ii) Aliingizwa kwenye ma**danguro** na ukahaba na kufunzwa kuweka pesa mbele. K.m. kisa cha James.

iii) Walimwengu walimchezea **hila.** – Hawa ni pamoja na Bi. Farashuu, Mama Jeni na Biti Kocho

iv) Alitarajiwa kufanya **kazi**. Biti Sururu alilalamika kuwa Maimuna alikuwa analala huku wenzake wanafanya kazi.

v) Maimuna alikosa jamaa yake. **Alilia** ndani kwa ndani alipowakumbuka/ Alitengana na jamaa yake.

vi) Alizama kwenye tabia ya **ulevi**.

vii) Mazingira alimoishi yalikuwa ma**chafu**. Kila mahali kulikuwa na mashimo, matope, uvundo wa vyakula panya na mende,kwa mfano kwa Mama Jeni na kwa Biti Sururu.

viii) Maimuna alijikuta kwenye maisha duni ya**ufukara**. Anapata chakula kwa hila kutoka kwa Ashuru. Anapewa samaki na Kabi.

ix) Alifanya kazi duni zenye **mapato** duni. Alihudumu kwenye vilabu kuuza tembo, kusafisha makopo.

x) Kwa sababu ya umri mdogo na urembo wake, watu hasa wenye pesa walimtumia kama **chombo** na kitega uchumi, kwa mfano alitumiwa kama kitega uchumi Rumbalola, Pumziko, Bobea.

xi) Alibobea katika **ukahaba**. (Kwa sababu ya urembo wake)

xii) Alijikuta kwenye maisha ya **uhuni** kama vile kung'ang'ania wanaume na kupigana k.m. Kijakazi.

xiii) Alikumbwa na matatizo ya jamii ambapo hakuna uhuru kamili, hakuna **mwongozo** wa maisha, jamii iko katika tanzo la kunyongwa. Alikosa mtu wa kumwelekeza

xiv) Alikumbwa na hali ya uhitaji na ufukara. K.m kukopa kwa **Ashuru**.

xv) Mapigo ya maisha yalimuumbua akapoteza urembo na kupata ma**kovu**/kukonda na kuchujuka.

xvi) Anapata dhiki ya kisaikolojia. Mwishowe kujiona **duni**/asiweze kuolewa. Anamwambia Kabi kuwa yeye ni mchafu.

xvii) Ulimwengu umembadilisha hadi akawa **fidhuli** kwa babake/ kukosa heshima. Anamkaripia na kumlaumu pale Bobea.

xviii) Kusingiziwa **wizi** na kufukuzwa kwa Mama Jeni.

xix) Ku**dharau**liwa / kudunishwa na watu, kwa mfano Farashuu/ Kijakazi/ Shoka.

**Zozote 10 x 2 = 20**

## MASHAIRI SEHEMU YA C

**4) KUJITEGEMEA**

a) Umuhumu wa nchi kujitegemea/ tatizo la mikopo na uombaji. ( **alama 2)**

b) Aina.

i) Tarbia – mishororo minne kila ubeti.

ii) Mathnawi – vipande 2 kila mshororo.

iii) Ukara – lina vina vya ndani vina na nje vinafanana/ urari

**Yoyote moja = 2 x 1 = 2**

c) Anashauri nchi

i) Kupata **wataalamu** wa ndani ya nchi kuendesha mambo.(ub. 4)

ii) Wananchi washiriki **kazi** za aina yoyote.(ub. 5)

iii) Wananchi waw**ajibike**. (ub. 2)

iv) Kuepuka na **mikopo** maana haina faida. (ub. 5)



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

v) Kujiepusha na **uzembe** (ub. 2/6)
vi) Wananchi wasitegemee vitu vya **bure**. (ub. 7/6)
vii) Kuzingatia **uongozi** wenye manufaa.(ub. 5)
viii) Wananchi waache kutegemea vya **ugeni**ni/ kujihoji. (ub. 3)
ix) Wananchi wa**saidia**ne. (ub. 3)

**Zozote 3 x 1 = 3 (za mwamzo 3)**

d) Inksari/ kufupisha (alama 2)

| | (ubeti) |
|---|---|
| wananchi | 3 |
| kupatakwe | 3 |
| pamwe | 5 |
| yalomakini | 5 |
| alotimiza | 6 |
| wongozi | 5 |
| twambizaneni | |

**au**

Kubananga/ kuboronga sarufi k.m.

Twaishije tujihoji (ub. 3)
Tongo tupangusaneni (ub. 3) – tupangusaneni tongo.
Mbele washike hatamu (ub. 4) - Washike hatamu mbele
Pamwe na nyingi imani (ub. 5) – pamwe na iimani nyingi
Shujaa itakiwavyo (ub. 7) – itakiwavyo shujaa
Kondo tusiamueni (ub. 7) – tusiamueni kondo

**Alama 5 x 1 = 5** **(tano za mwanzo)**

e) Shughuli zote za kiuchumi ziko mikononi mwa wananchi/ wakoloni pamoja na wanyonyaji wametengwa kando bila kitu/ kwa hivyo ni muhimu kufanya bidii maana hakuna njia nyingine ya kujiendeleza/ kwa kuwa daima/ siku zote mwombaji haheshimiki.[kila siku yeye ni mzembe (huzembea) na hukaa au husubiri kupewa – kusaidiwa]. **(alama 4)**

f) Ulaya, ng'ambo, nchi za nje, nchi za mbali, ugenini
Kufanana na, kuwa kama, mithili, kurandana, ja **(alama 2)**

## 5) HAKI

a) Ukosefu wa haki ulimwenguni/ jinsi haki inavyokosekana maishani. **(alama 2)**

b) Aina

i) **Tarbia** – mshororo minne kila ubeti.
ii) **Msuko** – kufupisha kwa mshororo wa mwisho
iii) **Ukawafi** – vipande vitatu mpangilio wa vipande vya mishororo (tatu)

**Yoyote 1 x 3 = 3. Taja 1 maelezo 2.**

c) **Tamathali**

i) **Tashihisi**/uhaishaji/ uhuishi – haki inazungumziwa kama binadamu/ haki inapewa wasifu wa kiumbe.
ii) **Tswira –** kwenye milima ilotueka, kupandia watu. – neno Haki.
iii) **Sitiari** -kiza/tatizonidaa –



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

iv) **Ritifaa** – kuzungumza moja kwa moja na kitu kisicho hai (Haki)

**Yoyote moja. Kutaja 1 maelezo 2 = 1 x 3 = 3**

**d) Idhini**

i) Matumizi ya msamiati usiokuwa wa kawaida/ **kuunda** – machumi (ub. 4)

ii) **Inkisari**; mbinu ya kufupisha maneno. Waloteuliwa (ub. 4) – walioteuliwa; litarajiwa (ub. 4) – lililotarajiwa; ilotueka – iliyotuweka; itavyopatika – itakavyopatikana; tukiifatia- tukiifuatia-tukiifuatia

iii) **Lahaja** – tukiifatia (ub. 5) – tukiifuatia; hichi (ub. 4) – hiki.

iv) **Tabdila** – kunaiyenea; akukumbukae; ilotueka

v) **Kuboronga sarufi** – sio hao mabwana (sio mabwana hao); na vikubwa visa (na visa vikubwa); kwenye hichi kiza (kwenye kiza hichi)

vi) **Utohozi** – tukisi **Tatu za mwanzo. 3 x 2 = 6**

e) Haki haifanyiki au haipatikani mahali penye mambo au visa vingi/ watu hawataki kufanya lolote la haki mradi watapata pesa/ sisi tunapata shida kubwa ila wao wako sawa/ haya ndiyo ya leo au siku hizi.
**AU** Watu wanapopatwa na shida/ mikasa/ taabu/ visanga hawatendewi haki/ ili kutendewa haki au kusaidiwa ni lazima walipe pesa [hongo]/ wakati wa shida hatuhurumiwi [hakuna utu, tunateseka bure, hawajali, hawana hisia/ Na huo ndio mtindo wa kisasa (na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi). **(alama 4)**

f) Maana ya maneno

i) Mahali palipo panatuumiza/ panatutesa/ dunisha/ turudisha nyuma.

ii) Kuweza kufikiri/ kusema/ kukubusu/ kutetea. **(alama 2)**

## MAYAI SEHEMU YA D

**6) Cheche**

**a)** Mbunda/ alikuwa anazungumzia nafsi yake/ akiwa amejibanza kwenye hoteli mjini/ akiwa anakumbuka tukio ambapo yeye pamoja na wanafunzi wenzake walipanga kuiteketeza shule yao ili kumpa funzo mwalimu mkuu kwa kuwadhibiti. Tukio hili lilisababisha hasara na vifo vingi. Matokeo haya ndiyo yaliyomfanya Mbunda kuungulika moyoni **(alama 4)**

**b) Chanzo**

i) **Utawala** mbaya/ ulegevu wa mwalimu mkuu (hakuchukua hatua za tahadhari)

ii) **Malezi** mabaya – mfano Mbunda anapodai hajawahi kuadhibiwa na wazazi.

iii) **Ubabe** unaotokana na fikira za ujana wa kupenda mambo yatendeke wanavyotaka. Uk. 126 ( …hawezi kutufanya mahabusu wake …)

iv) Madai ya wanafunzi ya **uhuru** mkubwa.

v) **Ukatili** wa wanafunzi wachache kupanga njama ya kuteketeza shule.

vi) Utovu wa **nidhamu**

**Nne za mwanzo 4 x 2 = 8**

**c) Matokeo**

i) Kuteketea kwa majengo ya shule/ uharibifu wa **mali**.

ii) **Vifo** vya wanafunzi 68.

iii) Kuvurugika kwa **utaratibu** wa shule.

iv) Athari za kim**hemko** kwa waliofika kusaidia au kushuhudia/ wengine hata walizirai.

v) Athari za kinafsia za walioteketeza shule/ **majuto** ya akina Mbunda, Musesi na hata Kamaliza.

vi) **Majonzi** kwa familia za waliokufa/ wananchi/ nchi.



Powered by: manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

vii) Watoto kutozikwa makwao kwa sababu ya kuchomeka na kutotambulika/ kuzikwa **kaburi** moja.
viii) **Majeruhi** – wanafunzi wajeruhiwa.
ix) Mwalimu mkuu ku**laumiwa** kwa uongozi mbaya.
x) **Jopo** kuundwa kuchunguza tukio hilo.

**Nne za mwanzo 4 x 2 = 8**

7) **Mganga**

i) Kutotambua umuhimu wa kuwapeleka watoto **shule**
ii) Kutumia **wembe** mmoja kuwachanja wagonjwa
iii) Hakuelewa **maendeleo**. Alipoenda mjini anaona jokovu kama sanduku la barafu.
iv) Hakufahamu chochote kuhusu **UKIMWI** na hakutaka kuuliza. Anasema ni ungonjwa wa mjini, unaosababishwa na kurukaruka
v) Hakujua jinsi ya kuji**tangaza**
vi) **Vifaa** alivyotumia havikuwa na maana. K.m. vibuyu, pembe, mbegu
vii) Kutumia **maneno** ambayo hata mwenyewe hayakuyaelewa
viii) Kutoa **tiba** ile moja kwa magonjwa yote na wateja wote
ix) Kutumia mimea bila kujali athari ki**mazingira**.
x) Kunyonya **damu** kwa imani kuwa anajiongezea
xi) Kutofahamu jina la mpira wa **kinga** wa ngono.

**Wateja**

xii) Kumwachia mganga **hela** za kununua nyembe ingawa wao ndio walioishi mjini/ Walishindwa au kudhibitisha upya wa nyembe anazotumia
xiii) Kumfuata mganga mbali kule **porini**/ badala ya kwenda hospitalini
xiv) Ni wasomi lakini walitafuta msaada wa mganga ili kupata **cheo**
xv) Kutofahamu ugonjwa waliougua hata ulipokuwa na **dalili** za wazi za UKIMWI
xvi) Kukubali ku**chanjwa** kwa wembe mmoja. Asteria na rafiki yake
xvii) Kutafuta **msaada** wa mganga kwa mambo kama vile mapenzi/ biashara/ ndoa
xviii) Kumpa mganga **maelezo** aliyoyatumia eti kuwagangua
xix) Imani kwenye **madoido** na mbwembwe za mganga.

**Kumi za mwanzo 10 x 2 = 20**

## FASIHI SIMULIZI . SEHEMU YA E.

a) Utani ni kipera cha Fasishi Simulizi chini ya uwanja/ utanzu wa mazungumzo Malumbano ya utani ni majibizano kati ya watu au makundi mawili kwa nia ya kutaniana. Hufanywa kwa kutumia maneno ya mzaha ili kuleta ucheshi. Utani ni utaratibu unakubaliwa na jamii. **(alama 2)**

b) Sifa za malumbano ya utani

i) Hutumia lugha ya **ucheshi**.
ii) Hutolewa kwa njia ya kudunisha/ **kejeli**
iii) Huwa na **mlengwa** mahsusi anayejulikana na anayetania/ anayetaniwa.
iv) Huwa na **kusudi** maalum inapotolewa.
v) Maneno yanayotumiwa yanaweza kuwa ya **aibu** au hayazingatii tauria.
vi) Lugha huweza kuwa ya **mafumbo/** tamathali za usemi.



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

vii) Baadhi ya kauli hutumia **fomyula**. K.m. katika jamii nyingi utani wa babu kwa mjukuu huwa. "Mke wangu, mbona leo ..."

viii) Katika kutaniana, wahusika **hujuana** na kuheshimiana/ mipaka hudumishwa.

ix) Kupiga **chuku**.

x) Hoja zozote **za mwanzo 4 x 2 = 8**

c) Umuhimu wa utani

i) Hujenga **mahusiano** kati ya wahusika/ umoja/ ushirika/ utangamano.
ii) Huchangamsha/ **huburudisha** wanaohusika.
iii) Huchemsha **bongo**.
iv) Hutia **ladha** mahusiano kwani huchekesha.
v) Huhifadhi **mila**/ utamaduni/ desturi/ itikadi/ kitambulisho cha jamii.
vi) Hufunza **maadili**.
vii) Hukosoa/ **huonya**.
viii) Kuendeleza **historia** ya jamii husika.
ix) Hukuza **lugha**.
x) Hu**elimi**sha jamii.
xi) Hutolewa kwa nia ya **kukejeli**.
xii) Hukuza **vipawa**.
xiii) Hujasirisha (**ujasiri**).
xiv) Kupitisha **wakati**
xv) Hukuza **ubunifu.** **Za mwanzo 5 x 2 = 10**



Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com